*JARIDA LA CHALUFAKITA*
*Juz. 5, 2023, 12-26*

# VIASHIRIA VYA UFUNGWA WA KISAIKOLOJIA KWA WAHUSIKA KATIKA RIWAYA YA KISWAHILI: MIFANO KUTOKA *VUTA N'KUVUTE NA KUFIKIRIKA*

Zuhura Ismail Said
Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima
saidzuhurat@gmail.com

na

Zuhura A. Badru
Chuo Kikuu cha Dodoma
badrulisajr@gmail.com

**Ikisiri**

*Makala hii imelenga kufafanua ufungwa wa kisaikolojia kwa kubainisha viashiria vyake katika riwaya teule. Nadharia iliyoongoza ukusanyaji, uchambuzi na uwasilishaji wa data za makala hii ni Nadharia ya Saikolojiachanganuzi. Aidha, usanifu uliotumika katika makala hii ni uchunguzi kifani. Makala hii ni sehemu ya utafiti uliofanyika kwa mahitaji ya kutunukiwa Shahada ya Uzamivu katika Chuo Kikuu cha Dodoma. Hivyo, data zake zilipatikana maktabani kupitia utafiti uliofanywa 2023. Data za maktabani zilipatikana kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa matini, hususani kusoma na kuchambua riwaya teule. Matokeo yanaonesha kwamba viashiria vya ufungwa wa kisaikolojia kwa wahusika katika riwaya teule vinadhihirika kupitia vilio, manung'uniko na uteti, hali ya unyonge na kukata tamaa na kufanya matendo yasiyo ya kawaida kwa wahusika wa kazi hizo.*

**Maneno muhimu**: *Viashiria, Ufungwa, Ufungwa wa kisaikolojia, Wahusika*

## 1.1 Utangulizi

Viashiria ni neno lililotokana na ishara likiwa na maana ya alama inayoelekeza jambo fulani (BAKITA, 2015). Kuwapo kwa alama hiyo kunasababisha kubainika kwa jambo fulani kamili. Kwa muktadha wa makala hii, dhana ya kiashiria ni mambo ambayo kuwapo kwake kuna sababisha ufungwa wa kisaikolojia ubainike. Viashiria vinaweza kubainika kupitia kauli ya mwandishi anapotumia nafsi ya tatu ya masimulizi ya hadithi. Pia, kupitia sauti au kauli zitokazo kinywani mwa wahusika kwa kuwakilishwa na nafsi ya kwanza. Hapa mwandishi huwabebesha kauli wahusika huku wakinung'unikia ufungwa wao. Nadharia ya Saikolojiachanganuzi imetumika kuwasilisha data za makala hii. Mihimili iliyotumika ni ule unaosisitiza kuwapo kwa mkufu wa viashiria katika kazi ya

kifasihi ambavyo mhakiki anawajibika kuvipa maana na misukumo ya ki-Freud ambayo ni matamanio, urazini na maadili.

Dhana ya ufungwa wa kisaikolojia inatokana na maneno mawili: ufungwa na saikolojia. Dhana ya ufungwa inatokana na neno "fungwa" lililotokana na kitenzi "funga" likiwa na maana ya kutokuwa huru au zuio la kufanya jambo fulani (TUKI, 2004). Dhana ya saikolojia kwa upande mwingine, ni stadi ya sayansi ya akili au nafsi ya mwanadamu na kazi zake hususani zile zinazoathiri mienendo katika mazingira maalumu (BAKITA, 2017). Hivyo, Ufungwa wa kisaikolojia ni ule msukumo wa ndani wa matamanio yanayoshindwa kutimizwa kwa sababu ya kani mbalimbali zinazotokana na asili au zisizo za kiasili (za kutengenezwa). Matamanio yanapofubazwa, husababisha nafsi ya mtu kushindwa kutimiza au kufanya mambo kulingana na matakwa yake kwa uhuru. Mwisho wake hamu ya kutimiza matamanio hayo hubakia ndani ya nafsi. Kani za asili zinazofubaza matamanio hayo ni kama vile; makatazo mbalimbali ya miiko ya kiimani na kimaadili kupitia kupitia vitabu vya dini au nguvu za mizimu kupitia wahenga. Kani zisizo za asili au za kutengenezwa husababishwa na makatazo ya kimamlaka yatokanayo na sheria, taratibu au mazoea yaliyojengwa na watu (Said, 2016, Said na Taib, 2019; Said, 2021).

Kimsingi, asili ya dhana ya ufungwa ilianza kujitokeza tangu Adam na Hawa[1] waliposhushwa kwenye bustani ya Aden na hivyo kufungwa kwa kutoruhusiwa kula tunda ambalo Mwenyezi Mungu aliwazuia. Kisa hiki kinaelezwa katika vitabu vitakatifu vya dini. Kwa mfano katika Kuran Tukufu (2:30-37) inaeleza kisa hicho kwa kusema: "Na kuleni humo popote mpendapo kwa starehe lakini msiukaribie mti huu tu; mkawa katika wale walio dhulumu". Pia, katika Biblia Takatifu, Kitabu cha Mwanzo 2:16-18 inasema: "Bwana Mungu akamwagiza huyo mtu, akisema, matunda ya kila mti wa bustani waweza kula, walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika". Kupitia maandiko haya, ni dhahiri kuwa dhana ya ufungwa imekuwapo tangu mwanzo wa kuumbwa kwa mwanadamu. Katika harakati za kutafuta uhuru wa matamanio, Adam na Hawa walijikuta wakimuasi Mwenyezi Mungu ili kutimiza uhuru uliominywa. Hali hii imeendelea kujitokeza zama hadi zama kwani watu wamekuwa wakifungwa katika miktadha mbalimbali.
Kwa jumla makala hii imejadili kuhusu viashiria vya ufungwa wa kisaikolojia katika riwaya ya Kiswahili kupitia riwaya mbili teule. Viashiria vimebainishwa

[1] Adam na Hawa/ (Eva) ni mwanaume na mwanamke ambao inasadikiwa kuwa ndio wanadamu wa kwanza kuumbwa na Mwenyezi Mungu na kuishi ulimwenguni katika bustani iitwayo Aden. (Kurani 2:30-36: 4:1 na Biblia Takatifu, Mwanzo; 2:16-18).

kupitia wahusika wa riwaya hizo. Wahusika ni vitu au watu ambao hutumiwa katika kazi za kifasihi ili kuwasilisha kweli inayopatikana katika ulimwengu halisi (Ntarangwi, 2004). Hivyo, mambo yanayowasilishwa na wahusika ni halisi, inawezekana yalitokea, yanatokea au yatatokea katika jamii. Hivyo, viashiria vilivyobainishwa katika makala hii ni kiwakilishi cha maisha halisi ya watu katika jamii. Mauki na Marandu (h.t)[2] wanafafanua kuwa, hivi sasa shida za kisaikolojia zimekuwa zikiwakumba watu wengi katika maisha ya kila siku na hivyo kuwasababishia msongo wa mawazo, kupata magonjwa ya akili na mwishowe mauaji. Maelezo haya ya Mauki na mwenzake yanabainisha tatizo kubwa la shida mbalimbali za kisaikolojia zinazotokana na watu kushindwa kutimiza matamanio yaliyomo kwenye nafsi zao. Hali hii inachangia watu wengi kuwa na msongo wa mawazo. Hii inatokana na jamii kushindwa kutambua mapema viashiria vya tatizo hili. Hivyo, kushindwa kutoa msaada unaohitajika kwa wakati. Kwa kuwa dhima mojawapo ya fasihi ni kufunza jamii na kuleta mabadiliko chanya, makala hii imetafiti viashiria vya ufungwa wa kisaikolojia ili kusaidia wanataaluma na jamii kwa ujumla kufahamu viashiria vya ufungwa huo ili kuchukua hatua sahihi mapema.

**1.2 Kiunzi cha Nadharia**

Nadharia iliyoongoza katika kukusanya, kuchambua na kuwasilisha data za makala hii ni Nadharia ya Saikolojiachanganuzi. Nadharia hii inaeleza jinsi masuala ya saikolojia yanavyoathiri utunzi wa mwandishi (Mulokozi, 2017; Wafula na Njogu). Kwa mujibu wa Wamitila (2002) na Msokile (1993), misingi ya nadharia hii iliwekwa na, Sigmund Freud (1856 - 1939) na kuendelezwa na Karl Jung (1875 - 1961) na Jacques Lacan (1901 - 1981). Ifuatayo ni mihimili ya Nadharia ya Saikolojiachanganuzi:

1. Kazi ya kifasihi ina mkufu wa viashiria, kwa sababu hiyo haina maana moja, hubadilikabadilika kutokana na kuwapo kwa mtelezo wa kiashiria kimoja hadi kingine katika mkufu wa uashiriaji. Neno moja linaweza kuelezewa kwa kurejelea jambo lingine. Kwa mfano, neno 'mwanamke' linaweza kurejelea mwanamume mwenye sifa za kike.
2. Kuna uhusiano wa msingi kati ya ishara na sababu za kutokea kwake.
3. Mhakiki wa kisaikolojiachanganuzi ana jukumu la kumsaidia msomaji au wasomaji kuelewa au kuhusianisha ishara na sababu za kutokea kwake.
4. Misukumo ya Kifreud ina nafasi kubwa katika nafsi ya mhusika, mtunzi, matini na hadhira inayopokea matini.
5. Mhakiki wa kisaikolojiachanganuzi afichue misukumo ya ki-Freud (matamanio, urazini na maadili) katika nafsi ya mhusika, mwandishi,

[2](h.t) haina tarehe

msomaji na andiko kupitia mkufu wa viashiria na kuhusianisha na kazi ya sanaa.

6. Mtunzi ametekwa nyara na mazingira anamoishi. Mhakiki wa kisaikolojiachanganuzi kupitia msukumo wa kimaadili, anaamini kuwa mwandishi ametekwa nyara na mazingira anamoishi. Hivyo, hayuko, na wala hatakuwa huru, hata kama angependa kuwa huru. Hii ni kwa kuwa utunzi wa kazi yake huathiriwa na jamii inayomzunguka.

Mihimili iliyoongoza uchambuzi wa data za makala hii ni mhimili wa kwanza hadi wa tatu. Aidha, msukumo wa matamanio ndio uliohusika zaidi kuchambua data za makala hii. Msukumo huu hubeba matamanio yote ya mtu bila kujali urazini wala itikeli za kijamii. Hii ni kwa kuwa kuna mfanano kati ya usanii na njozi zinazoashiria matumaini na matamanio. Hivyo, mihimili ya naddharia hii imetumika katika kuchambua data za makala hii kwa kubainisha matamanio ya wahusika katika kazi teule, kubaini viashiria, na kisha kuvipa maana.

**1.3 Methodolojia**

Data za makala hii zimepatikana kwa kutumia usanifu wa uchunguzi kifani. Usanifu huu hujihusisha zaidi na kuchunguza jambo fulani ili kutumia matokeo ya uchunguzi huo kama kiwakilishi cha kuonesha hali ilivyo katika jamii (Ponera, 2019). Usanifu huu umetumika ili kuchunguza kwa kina viashiria vya ufungwa wa kisaikolojia katika riwaya teule. Hivyo, ili kubainisha viashiria vilivyojitokeza katika riwaya hizo, mbinu ya uchambuzi wa matini ilitumika kuchambua riwaya mbili za *Vuta N'kuvute* (1999) na *Kufikirika* (1991). Riwaya hizi zimewakilisha riwaya zingine ambazo hazikutumika katika makala hii. Mkabala wa kitaamuli umetumika, kwa kuwa uwasilishaji wa data na mjadala wa makala hii ni wa maelezo.

**1.4 Muhtasari wa Riwaya Teule**

Kipengele hiki kinaeleza kwa ufupi muhtasari wa riwaya teule ili kuleta muumano wa kitaarifa.

**1.4.1 Muhtasari wa Riwaya ya *Vuta N'kuvute (1999)***

*Vuta N'kuvute* ni riwaya iliyoandikwa na Adam Shafi na ilichapishwa kwa mara ya kwanza mwaka 1999, na kampuni ya uchapishaji ya Mkuki na Nyota. Maudhui ya jumla katika riwaya hii ni ndoa za lazima za utotoni pamoja na harakati za kutafuta uhuru wa kisiasa. Katika riwaya hii, mwandishi anamtumia Yasmin kuwakilisha dhamira ya ndoa za kulazimishwa za utotoni. Anamwonesha Yasmin akiolewa na mwanaume mwenye umri sawa na wa baba yake mzazi pasi na ridhaa yake. Msimamo wa mwandishi katika riwaya hii ni wa kimapinduzi, na hivyo anaitaka jamii kubadili mitazamo ya kitamaduni iliyopitwa na wakati hususani ndoa za kulazimishwa. Aidha, kwa upande wa harakati za kisiasa mwandishi anamtumia mhusika Denge kupinga siasa za kikoloni.

### 1.4.2 Muhtasari wa Riwaya ya *Kufikirika (1991)*

*Kufikirika* ni riwaya iliyotungwa na Shaabani Robert na kuchapishwa kwa mara ya kwanza mwaka 1967 na kampuni ya East African Publishing House. Riwaya hii imepambwa na visa na matukio yenye ushikamani. Mwandishi amepanga visa na matukio ya sura ya kwanza hadi ya mwisho kwa kuendelezana. Kupitia kisa cha Mfalme kukosa mtoto, mwandishi anaonesha msimamo wa kutaka mabadiliko ya kifikra kwa kuegemea zaidi kwenye busara badala ya nguvu ya kimamlaka katika kufanya maamuzi na kutafuta masuluhisho ya matatizo ya jamii.

## 2.0 Viashiria vya Ufungwa wa Kisaikolojia kwa Wahusika katika Riwaya Teule

Sehemu hii imejadili viashiria vya ufungwa wa kisaikolojia. Mhimili wa Nadharia ya Saikolojiachanganuzi usemao kazi ya kifasihi ina mkufu wa viashiria ambavyo vinatakiwa kufafanuliwa na kupewa maana umetumika. Viashiria vya ufungwa wa kisaikolojia katika riwaya teule vimebainishwa, kujadiliwa na kupewa maana. Utafiti ulibaini viashiria vya ufungwa wa kisaikolojia katika riwaya teule ni kuwapo kwa vilio, kuwapo kwa manung’uniko, kuwapo kwa uteti, kuwapo kwa hali ya unyonge na kuwapo kwa matendo yasiyo ya kawaida. Hivyo, data hizo zinawasilishwa katika aya ifuatavyo:

### 2.1 Kuwapo kwa Vilio

Kwa mujibu wa Ali (2020), kilio cha hisia kinatokana na homoni nyingi za mfadhaiko. Husaidia kutuliza uchungu na maumivu ambayo mtu hupitia. Kimsingi, kina ishara ya mhusika kufungwa kwani kina ashiria hisia za ndani ambazo si rahisi mtu kuzibaini isipokuwa kwa ishara fulani kama vile kulia. Nadharia ya Saikolojiachanganuzi katika mhimili wake unaohusisha kuzipa maana ishara zinazobainika katika kazi ya fasihi, unasisitiza kuwa mtu anaposhindwa kutimiza matamanio ayatakayo hufidia kutimiza matamanio hayo kupitia njia mbadala. Miongoni mwazo ni kulia. Hivyo, data za utafiti wetu zimebainisha namna mhusika katika kazi ya kifasihi anavyolia kutokana na kufungwa na kushindwa kutimiza matamanio yake. Vilio vinajitokeza kama ifuatavyo:

Mwandishi katika riwaya ya *Vuta N’kuvute (1999)* ameonesha vilio mbalimbali kama ishara ya ufungwa wa kisaikolojia. Anasawiri kilio cha Yasmin alipokuwa akijilaumu kwa kuolewa na Bwana Raza; mwandishi anasema:

> Aliondoka mbele ya kioo na kuvaa nguo zake kwa haraka. Alipomaliza alijitupa kitandani na kulala kifudifudi na mara machozi yakaanza kumtoka. Zilimjia fikra za kwamba mtoto mzuri kama alivyo, mwenye mwili mzuri kama ule, leo anaishi maisha ya dhiki na unyonge vipi atakosa kupendwa na kijana

> mwenzake aliye mzuri kama yeye tena aliye Mhindi (Shafi, 1999:21).

Nukuu hii inaonesha namna Yasmin anavyolia na kutoa machozi ya hisia kali kama kiashiria cha ufungwa wa kisaikolojia unaomkabili. Katika muktadha huu, kilio kinabainisha kuwapo kwa ufungwa wa kisaikolojia uliotokana na mila na desturi za jamii. Ufungwa huu wa kisaikolojia ndio unaosababisha Yasmin alie kwani hii imeonesha kuwa matamanio ya nafsi yake yamefungwa kitamaduni na hivyo hayupo huru kumchagua mpenzi amtakaye. Msukumo wa Ki-Freudi wa kimaadili unamwekea mipaka ya uhuru wake na hivyo anashindwa kuwa huru.
EATV (2018)[3] katika ukurasa wao wa kimtandao wanaeleza kuwa kuna faida nyingi za kulia zikiwamo za kimwili na kiakili. Wamefafanua kuwa kulia kunasaidia kuondoa msongo wa mawazo. Hii ni kwa kuwa, machozi yana kiwango kikubwa cha madini ambayo husaidia mliaji kujisikia ahueni baada ya kumaliza kulia. Mwandishi katika makala hiyo anasisitiza kuwa watu wanapaswa kulia wanapopata shida mbalimbali hasa za kisaikolojia. Anadokeza kuwa, kuzuia kulia kunaweza kuongeza viwango vya shida na kusababisha magonjwa. Kilio cha mhusika Yasmin katika riwaya ya *Vuta N'kuvute* kinampa ahueni kiasi kwamba anapata ujasiri wa kujikomboa na ufungwa huo na hatimaye anamtoroka Bwana Raza na kuwa huru.

Freud anadai kuwa nafsi ya matamanio inapokabiliana na msongo wa mawazo, kulia kunaweza kuwa suluhisho au njia ya kuondoa mrundikano wa mawazo na kusaidia nafsi ya urazini kudhibiti hisia. Suala la kulia katika jamii zetu limekuwa likifanywa na watu wengi katika miktadha tofauti. Kwa mfano, mtoto hulia akikitaka kitu, kulia kwake huwa kunatupa ishara kuwa labda ana njaa, anaumwa au anahisi joto ama baridi. Kwa upande mwingine, watu wazima hulia kwenye misiba na wakati mwingine hulia wakiwa na furaha au huzuni. Kulia huweza kuwa ni tiba kwa mtu aliyepatwa na huzuni kwani anapomaliza kulia anaweza kuongea na kupumua vyema zaidi. Hii ni sawa na asemavyo Clemence (2017) kwamba, miongoni mwa faida za kulia ni kusaidia kupunguza na kuondoa maumivu ya kihisia kama vile msongo wa mawazo, hasira na wasiwasi. Hii ni kwa kuwa mtu anapolia huruhusu kutoa hisia zake na kumwacha akiwa amesafishika kiakili.

### 2.2 Kuwapo kwa Manung'uniko na Uteti

Suala la manung'uniko na uteti limejadiliwa katika riwaya teule. Matokeo ya utafiti yanadhihirisha hili kama ifuatavyo:

---

[3] Imesomwa katika ( https://www.eatv.tv/sw/news) (imepitiwa tarehe 3 Sept, 2023 saa 5:26 mchana).

### 2.2.1 Manung'uniko

Manung'uniko ni kiashiria kimojawapo cha ufungwa wa kisaikolojia. Neno hili linalotokana na neno nung'unika likiwa na maana ya kulalamika kwa sauti ya chini chini kuonyesha kutoridhika na jambo fulani (BAKITA, 2015). Waandishi wanasawiri dhana hii katika riwaya teule. Kwa mfano, katika riwaya ya *Vuta N'kuvute* mwandishi ameonesha kiashiria cha manung'uniko kwa mhusika Yasmin. Mwandishi anamuonesha namna mhusika huyo anavyotamani kuwa na nguo za kutokea lakini hana na hivyo kujikuta akinung'unikia hali yake. Mwandishi anasema "Kwa sauti ya unyonge Yasmin alijibu, ah! Hata nikitaka, cha kukivaa sina, nguo zangu ndo hizi hizi,…" (uk. 36). Kauli hii inaonesha kuwa Yasmin amefungwa kisaikolojia kutokana na dhiki na uchumi duni alionao. Nadharia ya Saikolojiachanganuzi inaeleza kuwa kunung'unika kunaweza kuwa ishara mojawapo ya mgongano kati ya nafsi ya matamanio na nafsi ya urazini ambayo huweka bayana madhara yatakayotokea endapo nafsi ya matamanio italazimisha kufanya mambo kwa utashi wake. Freud anaona kunung'unika au kulalamika kunaweza kuwa njia ya mtu kutoa nje hisia au kero zisizotatuliwa kutokana na shinikizo la matakwa ya kijamii na maadili.

Vilevile, kiashiria cha manung'uniko kimejitokeza katika riwaya ya *Kufikirika* ambapo mhusika Mfalme ananung'unikia suala la ugumba alilokuwa nalo pamoja na malkia wake. Mwandishi anasema:

> Ustawi uliofanyika katika nchi hii tangu mwanzo wa ufalme wangu umeniletea heshima, lakini ugumba umemeza heshima yangu na utasa umetia vumbi fahari ya malkia. Sina mtoto wa kurithi kiti changu na ufalme, kutoa mashauri ya hekima barazani kama mababu zake, kuongoza watu katika vita, kuvuta tumbaku katika kiko changu na kunywa kwa bilauri imfanyayo mnywaji wake kuwa msemaji mwema mbele ya hadhara ambayo mimi nimerithi kwa wazee wangu (Robert, 1991:3).

Kauli hii ya Mfalme ni ya manung'uniko kwani anajiona si sawa kwake kukosa mtoto hasa ukizingatia nafasi yake katika nchi ya Kufikirika. Mfalme amefungwa kisaikolojia kutokana na na jaala ya Mwenyezi Mungu ya kutompatia mtoto. Matamanio ya Mfalme yalifubazwa na jaala hiyo na hatimaye kuishia kunung'unikia ufungwa huo. Hata hivyo, katika kukwepa ufungwa huo, Mfalme anaamua kupindisha sheria kwa kutoa kafara kwa kumwaga damu ya mtu. Mfalme alikiuka sheria ili kutimizia matamanio na mahitaji ya nafsi yake.

Kitendo cha Mfalme kutamani mtoto hadi kumwaga damu kinaakisi maisha halisi ya jamii. Mwanadamu hutamani maisha mazuri kama vile kumiliki nyumba, magari, wake na wanaume wazuri, lakini kutokana na kuwa na uchumi mdogo, matamanio haya hufubazwa na hivyo kumfanya binadamu aishie kunung'unika.

Freud anadai kuwa matamanio ya mtu yasipotimizwa kwa wakati, matamanio hayo hudhihirika kupitia mitelezo ya kauli. Hii ni kusema kuwa matamanio yanapowekewa mipaka ya kutimizwa kwake, hutimizwa kupitia njia zingine kengeushi kama vile manung'uniko, vilio na hata matusi. Naye George (2022) anaeleza kuwa sababu za mtu kuwa na manung'uniko ni pamoja na kutopata alichotarajia kwa wakati, kuchoshwa na hali aliyopitia kwa kipindi fulani, na kuhisi kwamba ameachwa au kutengwa na Mungu. Maelezo haya ya George yanalandana na hali ambayo Yasmin alikuwa nayo kutokana na changamoto za kiuchumi (uk 36). Hii ina maana kwamba kama Yasmin angekuwa vizuri kiuchumi angeweza kujinunulia mavazi na kisha kutimiza hitaji lake.

### 2.2.2 Uteti

Uteti ni sehemu ya manung'uniko kwani inapotokea mtu akanung'unika aghalabu kinachofuatia ni uteti. Neno uteti limetokana na neno teta. BAKITA (2015) linafasili neno teta kuwa ni kumsemea maneno ya uongo mtu akiwa hayupo na bila yeye kujua unalosema. Kwa jumla, dhana ya uteti katika makala hii inarejelea mazungumzo ya mhusika mmoja au zaidi kumsema mhusika fulani ambaye hayupo kwenye mazingira waliyopo. Maneno hayo huweza kuwa mambo ya kweli au yasiyo ya kweli. Suala hili linajidhihirisha katika riwaya ya *Vuta N'kuvute* ambapo Yasmin anamteta Bwana Raza kwa rafiki yake, Mwajuma kwa kusema:

> "… baba lenyewe lina wivu kama nini …" "Ah babu we unajua maneno ya mume wangu tena akianza hamalizi" "Ah shoga yangu we yasikushughulishe! Hiyo ndiyo desturi ya wanaume wazee wanaooa wanawake watoto wadogo, basi maneno yake usiyajali."… Ah! yule alikuwa si mume wa kumtaka mimi mwenyewe, niliozeshwa tu na wazee wangu na mimi sikuweza kuwavunja". Alisema Yasmin akitabasamu na kuonyesha meno yake yaliyokuwa yaking'aa kama marmar (Shafi, 1999:23).

Kimsingi, nafsi ya matamanio inawakilisha tamaa za msingi za mtu, kama vile haja ya chakula, ngono, na raha. Kwa hivyo, inapotokea mtu kuhisi hasira au wivu kwa mtu mwingine, nafsi ya matamanio inaweza kumsukuma kumuumiza ili kupata raha na kupunguza machungu na hasira kwa mtu husika. Nukuu hiyo inaonesha jinsi nafsi ya matamanio ilivyomsukuma Yasmin na Mwajuma kumteta Bwana Raza ili kujipunguzia uchungu. Hii inadhihirisha kuwa yote yanayofanywa na Bwana Raza, Yasmin alikuwa haridhishwi nayo isipokuwa tu kwa kuwa tamaduni zilimlazimisha awepo kwenye ndoa hiyo. Hivyo, kwa kuwa nafsi ya matamanio ilikuwa na nguvu kushinda nafsi zingine, zilimsukuma afanye hivyo. Hata hivyo, Yasmin alijinasua kutoka katika ufungwa huo wa kitamaduni kwa kumkimbia Bwana Raza. Uteti pia unajitokeza pale Mwajuma na Yasmin wanapomteta Shihab kutokana na wivu wake kwa mke wake Yasmin. Mwanandishi anasema:

> ...Umekonda shoga yangu" "Nisikonde mwanaume yule ana wivu, ana gubu, nongwa, kama mwanamke" Yasmin alilalamika. Nakuambia kaniweka ndani kama mwari, hata huyo mwari ana afadhali, sina shoga, sina jirani sina jamaa mimi na ndani na ndani na mimi sendi sirudi." Bwana yule mgonjwa sasa anakufungia ndani kwani yeye kakukuta wapi? Kakukuta unatawishwa si kakukuta unabembea na maisha tena kwa mapana na marefu. Babu wee utafikiri siye aliyenikuta katika taarabu nikistarehe na vijana wenzangu". Mazungumzo juu ya wivu wa Shihab ndiyo yaliyokuwa yametawala kikao chao, wakamsema mpaka wakachoka... (Shafi, 1999:211).

Katika nukuu hii inaonesha namna nafsi ya matamanio ya Yasmin ilivyotamaani Shihab aachane na wivu.Wivu wa Shihab kwa Yasmin ulikuwa unamnyima raha. Kwa kuwa Yasmin hakupenda wivu wa Shihab, alijikuta akijiliwaza kwa kumteta. Hii inahusishwa na mchakato wa kisaikolojia. Inapotokea nafsi ya matamanio kutamani jambo fulani na ikiwa jambo hilo halikubaliwi na nafsi ya urazini, urazini hutoa suluhu nyingine ambayo haina madhara kwa nafsi ya matamanio.

Vilevile, kiashiria cha uteti kinadhihirika katika riwaya ya *Kufikirika* kupitia wanachama wa baraza kulazimishwa kuahirisha sheria ya kuruhusu kafara ya damu ya mwanadamu ili kukinga maisha ya mtoto wa Mfalme wa Kufikirika. Kutokana na agizo hili wanachama wa baraza wanaanza kunung'unika na kuteta wakiwa katika kikao. Kama mwandishi anasema:

> Alikaa kitako kwa makuu kama msemaji aliyetumaini kuwa hotuba yake itatenda yote aliyoyataka: lakini ilikuwa sivyo kabisa. Hotuba hii ilizizimisha damu katika mishipa ya wanachama wengi wa baraza. Wanachama walinong'onezana. "Ubora ni kubadili mabaya kwa mema, siyo mema kwa mabaya!
> (Robert, 1991:35).

Nukuu hii inaonesha minong'ono ya wajumbe wa baraza wanaolazimika kutenda kinyume na matamanio yao ili kumsitiri mfalme wao. Mwandishi anaeleza namna wajumbe wa baraza walikuwa wamepigwa butwaa na maamuzi ya Mfalme. Wananchi wake walimuamini kutokana na huruma yake. Kutokana na hamu ya kupata mtoto, Mfalme aliliamuru baraza kupindisha sheria ili waruhusu kutoa kafara ya damu ili apate mtoto. Hali hii iliibua minong'ono kwa wanachama wa baraza. Kuwapo kwa minong'ono iliyojitokeza kwa wanachama ni dhahiri kuwa maamuzi na maagizo yaliyotolewa mbele ya baraza hayakukubaliwa na wanachama.

George (2022) anapoeleza sababu ya kusengenya ni mtu kukosa kitu kinachotamaniwa huku watu wengine wakiwanacho. Maelezo haya ya George hayapishani na fikra za Nadharia ya Saikolojiachanganuzi isemayo mwandishi

ametekwa nyara na mazingira anayoishi hivyo hawezi kuwa huru hata angetaka. Mhimili huu unatuelekeza kusema kuwa wanachama wa baraza hawakutaka kuruhusu kupindishwa kwa sheria ya kutoa kafara kwa kumwaga damu. Lakini hawakuweza kwa sababu hawako huru. Hivyo nafsi zao za matamanio hazikuridhika na uvunjaji wa sheria hiyo, hivyo waliyatoa kwa njia ya manung'uniko. Freud (1901) anaona kuwa matamanio yaliyofichika huwasilishwa kwa ndimi za kauli. Anaamini kuwa ndimi za kauli hutokana na mvutano kati ya mawazo yaliyokandamizwa, matamanio au wasiwasi, na sheria za kijamii au hali iliyopo ambayo akili hujaribu kuidhibiti. Mawazo haya ya Freud yanafafanua namna ambavyo mawazo yaliyojificha yanaweza kuibuliwa kwa njia mbalimbali ikiwamo manung'uniko.

**2.3 Hali ya Unyonge**

Unyonge ni hali ya huzuni anayoipata mtu kutokana na maradhi, upweke, umasikini au uchovu wa kazi (BAKITA, 2017). Aghalabu, mtu mwenye unyonge hukabiliwa na shida mbalimbali ndani ya nafsi yake hasa zitokanazo na upweke chambilecho BAKITA. Wahusika katika riwaya teule wamekuwa na hali ya unyonge kwa namna mbalimbali. Unyonge uliojitokeza kwa wahusika hao umetokana na upweke, umasikini na hata maradhi. Kwa mfano, katika riwaya ya *Vuta N'kuvute* mwandishi anaonesha hali ya unyonge kwa Bwana Raza na Yasmin. Hali hii imetokea baada ya Yasmin kulazimishwa kuolewa na mume ambaye hamtaki na hivyo kila mmoja kujikuta akikosa furaha katika ndoa hiyo. Mwandishi anasema:

> Bwana Raza hakuwa na raha ya kuwa na mke na Yasmin hakuwa na raha ya kuwa na mume. Maisha ya watu wawili hawa yalikuwa ya bahati nasibu na hakuna mmoja kati yao aliyekuwa na raha na hali hiyo ilimfanya Yasmin kuondokea na tabia ya unyonge akiona kama dunia imemwonea kuozeshwa mume asiye makamo yake wala asiyemvutia hata kidogo (Shafi, 1999:4).

Maelezo haya yanasawiri wahusika wote wawili wakijikuta wakikosa furaha katika ndoa yao. Hali hii ya unyonge inawasababishia kukata tamaa na kuwa na fikra za chuki juu ya ndoa. Nadharia ya Saikolojiachanganuzi inamwelekeza mhakiki wa kazi ya fasihi kuchunguza nafsi za wahusika ili kubaini dhamira za ndani za nafsi za wahusika hao. Nukuu ya hapo juu inaonesha kuwa matamanio yao ya kuishi kwa furaha katika ndoa yao hayakufikiwa. Hata hivyo, walilazimika kukaa katika ufungwa huo mpaka Yasmin alipoamua kuutafuta uhuru wake kwa kutoroka.

Pia, hali ya unyonge imejitokeza kwa mhusika Bukheti ambapo mwandishi anaeleza namna mhusika huyo alivyokosa furaha baada ya kulitamani penzi la Yasmin. Hii ni baada ya Yasmin kutoroka kwa Bwana Raza. Mwandishi anasema:

> Kama uchangamfu uliokuwemo ndani ya nyumba ya Yasmin ndio uliofika mpaka kwa Bukheti ukamchangamsha na yeye, unyonge uliomo mle hivi sasa uliiambukiza nyumba yake naye akawa hana furaha (Shafi, 1999:39).

Unyonge wa Bukheti ni kiashiria cha ufungwa wa kisaikolojia kutokana na matamanio yake ya kuwa karibu na Yasmin kutotimizwa. Aidha, mwandishi anamsawiri mhusika Yasmin kwa kuonesha namna alivyokata tamaa ya maisha kwa kukataliwa na ndugu zake wote kiasi cha kusaidiwa na Denge aliyekuwa mtu baki. Mwandishi anasema:

> Denge huwezi kunisaidia, hata ukitaka kunisaidia hutoweza. Hapa unaponiona sina mbele wala sina nyuma walio wangu wamenitupa na kunikataa kama kwamba siwahusu ndewe wala sikio. Hapa unaponiona nilikuwa nafikiri kwenda kumtazama mama yangu lakini natia nikitoa, sijui nende au nisende (Shafi, 1999:70).

Maelezo haya ni kiashiria cha ufungwa wa kisaikolojia kwa Yasmin baada ya matamanio yake ya kukubaliwa na mama yake kutofikiwa. Katika maisha halisi ni matamanio na matarajio ya kila mtu kukubaliwa na watu wake wa karibu hasa mama yake. Hivyo, inapotokea hata mama mzazi anashindwa kujali na kumkubali mtoto wake basi ni rahisi sana mtu anayekataliwa kukata tamaa na kuona maisha hayana maana.

Kiashiria cha unyonge kinapatikana pia katika riwaya ya *Kufikirika* ambapo mfalme na malkia wake wanakosa mtoto takribani miaka tisa. Mwandishi anasema:

> Siku za ujana wetu zinapungua upesi sana, karibu tutaingia katika uzee na kupotea katika giza la mauti bila ya matumaini ya kupata mtoto wa kuwa nguzo ya nyumba ya ufalme wa Kufikirika (Robert, 1991: 5).

Hotuba hii ya mfalme mbele ya baraza katika jitihada za kutafuta msaada wa ushauri inaonesha dhahiri hali ya unyonge, majonzi, huzuni na kukata tamaa kwa mfalme. Katika hali halisi kuna matarajio na matamanio kuwa mtu, aghalabu, mfalme anapofariki arithiwe na watoto wake. Inapotokea matamanio hayajatimizwa mtu huyo huingia katika ufungwa wa kisaikolojia na hata kuona maisha yake hayana maana. Hali ya namna hii isiposhughulikiwa mapema huweza kuishia katika madhara makubwa kwa mhusika. Nadharia ya Saikolojiachanganuzi inaeleza kuwa inapotokea matamanio hayakidhiwi, nafsi ya matamanio huendelea kusukuma kusudi kuyafikia. Hii inaweza kusababisha hisia za kukosa kuridhika, kuudhika, na hata hasira, ambazo zote zinaweza kuchangia unyonge. Hivyo, ni muhimu watu kubaini viashiria vya ufungwa wa kisaikolojia hususani wanapoona

watu wamekuwa katika hali ya unyonge ili kutoa msaada wa haraka wa kisaikolojia unaotakiwa.

**2.4 Kufanya Matendo Yasiyo ya Kawaida**

Matendo yasiyo ya kawaida kwa mujibu wa makala hii ni matendo yanayopingana na matarajio ya jamii au ya mtu binafsi. Kwa maneno mengine, ni matendo ambayo yanayotoka nje ya mfumo wa kawaida. Matendo hayo aghalabu yanayopingana na matarajio ya jamii au ya mtu binafsi. Hiki ni kiashiria cha ufungwa wa kisaikolojia kilichobainika katika riwaya teule ambapo baadhi ya wahusika walibadilika kimatendo na kihisia.

Katika riwaya ya *Vuta N'kuvute* mwandishi anamsawiri mhusika Denge akifanya tukio lisilo la kawaida la kutoroka akiwa kwenye genge[4] la kuchimbua mawe ili kutosheleza matamanio yake ya kuwa huru. Anaamua kuukimbia ufungwa wa kisaikolojia uliokuwa ukimkabili kama inavyonukuliwa katika dondoo lifuatalo:

> …"Afande" alimwita "Unasemaje"? Naomba kwenda haja ndogo." Haya nenda, haraka urudi sasa hivi," alimruhusu, viwingu vidogo vidogo vya moshi wa sigareti vikipepepruka kutoka mdomoni mwake…. Alikuwa kama mwizi wasiwasi umemjaa akahisi kama watu wote duniani wanamwangalia yeye vile anavyotambaa na mashahidi pekee waliyokuwa wakiyashuhudia aliyokuwa akiyafanya ni vichaka vilivyomzunguka (Shafi, 1999:270-274).

Nukuu hiyo inaonesha mbinu za Denge za kutaka kutoroka. Mara tu baada ya kuruhusiwa kwwenda kujisaidia hakurudi tena. Tukio la Denge kuamua kutoroka gerezani linahusishwa na nafsi ya matamanio. Nafsi hii inawasilisha tamaa za msingi za mwanadamu, kama vile kutaka raha na kuepuka maumivu. Inaweza kutafsiriwa kuwa nafsi yake ya matamanio ilitamani uhuru na kuyakwepa maumivu wanayopata wafungwa wakiwa gerezani. Si jambo la kawaida kwa mfungwa kutoroka gerezani lakini kutokana na ufungwa wa kisaikolojia uliokuwa ukimkabili, nafsi yake ilisukumwa kutoroka. Kitendo cha Denge kuamua kutoroka ni kiashiria cha ufungwa wake. Inaonesha wazi hakuwa huru wala kuyaridhia maisha ya gerezani. Hivyo matamanio yake yalihitaji kuwa huru na aondokane na ufungwa uliyokuwa ukimkabili.

Vilevile, katika riwaya ya *Kufikirika* tabia ya kufanya matendo yaasiyo ya kawaida ilijitokeza kwa mhusika Mfalme ambaye alikuwa na tabia ya ukarimu na upole lakini alijikuta akifanya maamuzi yasiyo sahihi ya kupindisha sheria ili atimize hitaji lake la kupata mtoto. Hamu ya mfalme kupata mtoto lilimbadilisha kutoka

[4] Ni maeneo maalumu ambayo wafungwa huenda kufanya kazi wanazopangiwa (Said, 2016).

kwenye matendo yake ya upole na kuwa na matendo ya ukatili kwa wananchi wake. Hali hii ilisababisha aende tofauti na sheria za nchi yake. Katika ukurasa wa 32 mwandishi anasema "Mimi mwenyewe nachukia sana kafara hili kama sheria za nchi zichukiavyo, lakini sina jambo jingine la kutenda". Kauli hii ya mfalme inaonesha wazi kuwa amefungwa kisaikolojia kwa suala la kutopata mtoto na kwa sababu hiyo yuko radhi kufanya chochote ili mradi mtoto apatikane. Mtu aliye katika ufungwa wa kisaikolojia anaweza kufanya jambo lolote hata lile la kuvunja maadili na utu ili mradi atimize matamanio ya nafsi yake. Adam (2014) anadai kuwa, mwanadamu anatawaliwa zaidi na matamanio kwa sababu ndiyo huchukua nafasi kubwa katika maisha ya mwanadamu. Katika harakati za kutimiza matamanio hayo mwanadamu hujikuta akijiumiza yeye mwenyewe au watu wengine wanaomzunguka.

**2.5 Hitimisho**

Kwa ujumla, uchunguzi wa makala hii umeonesha jinsi waandishi Shaaban Robert na Adam Shafi walivyotumia viashiria vya ufungwa wa kisaikolojia kwa wahusika katika riwaya teule. Viashiria hivyo ni vilio, manung'uniko, uteti, hali ya unyonge na wahusika kufanya matendo yasiyo ya kawaida. Kwa mfano, mwandishi amemsawiri mhusika Yasmin namna alivyolia kuonesha matamanio yake ya kuwa na mwanaume wa rika lake. Isivyo bahati wazazi wake walimlazimisha kuolewa na Bwana Raza ambaye alikuwa sawa na baba yake. Hali hii ilimtia majonzi na hivyo iliashiria ufungwa wa kisaikolojia alionao. Pia, manung'uniko ya Mfalme wa Kufikirika yalionesha ufungwa wa kisaikolojia kwake. Alitamani mtoto lakini kutokana na jaala hakuweza kupata mtoto kwa wakati alioutaka Halikadhalika mhusika Yasmin na Mwajuma walimteta Bwana Raza wakilalamikia tabia yake ya kuoa mtoto mdogo ambaye angeweza kumzaa. Pia, hali ya unyonge iliashiria ufungwa wa kisaikolojia kwa wahusika Bwana Raza na Yasmin kwa kukosekana kwa amani katika ndoa yao. Wahusika wengine waliokutwa na kiashiria hiki ni Bukheti na Mfalme wa Kufikirika. Aidha, mhusika Mfalme alijikuta akitenda matendo yasiyo ya hulka yake kwa sababu alitamani kupata mtoto kwa namna yoyote.

Kutokana na viashiria vilivyochunguzwa katika riwaya teule inatukumbusha kuwa ufungwa wa kisaikolojia unaweza kuwa na matokeo mabaya kwa wahusika na jamii. Hivyo, kugundulika kwa viashiria vya kisaikolojia mapema inaweza kupunguza madhara ya ufungwa huo. Aidha, mjadala wa makala hii unatoa wito na mwaliko wa ushirikiano baina ya wanataaluma, watunzi wa kazi za fasihi, walimu, wazazi, walezi, wanasaikolojia na jamii kwa ujumla kuwa na mijadala ya pamoja inayohusiana na mada inayojadiliwa, kusudi kupeana maarifa juu ya jambo hili. Hii itasaidia kutoa mchango katika ujenzi wa fasihi na maisha bora kwa mtu mmojammoja na jamii nzima.

**Marejeleo**

Ali, H. (2020). Hizi hapa faida za machozi mtu anapolia kwa mujibu wa utafiti. https://kiswahili.tuko.co.ke/355475-machozi ni muhimu sana fahamu yake katika afya ya binadamu.html (imepitiwa tarehe 3 sept, 2022 saa 6:51 mchana).

Adam, O. A. (2014). *Kuchunguza Dhamira za Kijamii na Kitamaduni katika Riwaya ya Kiswahili: Mifano kutoka Kuli na Vuta N'kuvute.* (Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu katika Fasihi ya Kiswahili). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

BAKITA, (2017). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers (Ltd).

BAKITA, (2015). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*, Nairobi: Longhon Publishers.

Biblia Aagano la Kale, (https://somabiblia.com/biblia-kwa-kiswahili-na-kiingereza-download/) imepitiwa tarehe 16/11/2022 saa 8:15 mchana)

Clemence, N.J, Zijue Faida za Kulia, (*Saikolojia*, JUNI 13, 2017). imesomwa katika https://m.facebook.com/saikolojia/ tarehe 18.7.2023, saa 7:35 mchana.

Farsy, A. S. (1993). Quran Takatifu. Nairobi: Islamic Foundation.

George, L (2022) Sababu za Manung'uniko. Imesomwa katika http://www.seggahgtz.com/ (Imepitiwa tarehe 15 Septemba, 2023).

Mauki, C na Marandu, D. (h.t). *Msongo wa Mawazo: Uelewe na Umudu.* Dar es Salaam: Kiwonyi Printers and Media Publishers.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi. East African Education Publishers.

Mulokozi, M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU.

Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Rock Island: Augustana College.

Ponera, S. A. (2019). *Misingi yaUtafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasnifu*. Dodoma: Central Tanganyika Press.

Said, Z. (2016). Usawiri wa Ufungwa katika Riwaya za Kiswahili: Mifano kutoka katika riwaya ya *Umleavyo* na *Haini*. Tasnifu ya Shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili (Haijachapishwa). Dodoma: Chuo Kikuu cha Dodoma.

Said, Z. I., (2021). "Ufungwa wa Kisaikolojia katika Riwaya ya Takadini" *Ruaha Catholic University, Journal of Education and Development* (*RUCUJED*), Volume 1, Issue 2, (197- 2016)

Said, Z., & Taib, A. H. (2019). *Fasihi ya Ufungwa: Nadharia na Mikabala Uhakiki kama Kifani1*. Dar es Salaam: Heko Publisher.

Robert, S. (1991). *Kufikirika*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

Shafi, A. S. (1999), *Vuta N'kuvute, Dar es Salaam:* Mkuki na Nyota Publishers.

TUKI, (2004). *Kamusi ya Kiswahili sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.

Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Kenya Phoenix.

Zifahamu Faida za Kulia , 6TH JAN , 2018. Imesomwa katika (https://www.eatv.tv/sw/news/current-affairs/zifahamu-faida-za-kulia (imepitiwa tarehe 3 Sept, 2022 saa 5:26 mchana).